

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

مشروع تَعَلُّم الإسلام – ما هو الإسلام – اللغة السواحلية

Somo la 4

الدرس الرابع

IBADA KATIKA UISLAMU

Haikubaliki ibada yoyote ile katika Uislamu isipokuwa itekelezwe kwa ajili ya Allah tu na iende sambamba na alichokuja nacho Mtume Muhammad -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-

Swala kwa mfano, hii ni ibada ambayo haitekelezwi ila kwa ajili ya Allah, na haiwezi kuwa sahihi isipokuwa itekelezwe kwa kufuata utaratibu alioubainisha Mjumbe wa Allah -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-

Na hilo lina sababu zake, nazo ni:

1. Allah aliamrisha ibada itekelezwe kwa Ikhlasi ya kuabudiwa yeye tu, akiabudiwa mwingine pamoja na Allah huko ni kumshirikisha, Allah anasema: **“Muabuduni Allah na wala msimshirikishe na chochote kile”** [Nisaa 36].
2. Allah –Mtukufu alietakasika na mapungufu- ndie aliehusika kuweka sheria, kwa hiyo ni haki yake peke yake, na atakae abudu kupitia sheria ambazo hakuziweka Allah huyo atakuwa amemshirikisha Allah kwenye uwekaji sheria.
3. Allah ametukamilishia dini, hivyo basi yule ataevumbua Ibada yake, huyu atakuwa ameituhumu dini kuwa ina mapungufu.
4. Lau ingekuwa kila binadamu inafaa kufanya ibada aitakayo kwa muundo autakao, basi kila mmoja angekuwa na utaratibu wake maalum wa kufanya ibada, kwa kule kutofautiana tabia na mienendo yao.

NGUZO ZA UISLAMU

Nguzo za Uislamu ambazo Allah ameziamrisha ni tano:

1. Kushuhudia yakwamba hapana apasae kuabudiwa isipokuwa Allah na hakika Muhammad ni mjumbe wa Allah.
2. Kusimamisha Swala.
3. Kutoa Zaka.
4. Kufunga Ramadhani.
5. Kuhiji Nyumba ya Allah.

KITU GANI UISLAM UNATAKA KWETU?

Uislam haumtaki Muislam aiache dunia kabisa, wala haumtaki akae Misikitini tu ili afanye Ibada, au akae kambi ya kivita tu ili kuutetea Uislam, siyo hivyo! Bali Uislam unataka Waislam wawe wenye maendeleo bora, wawe mabwana walioendelea, na kiuchumi wawe matajiri zaidi, na kielimu wawe wasomi zaidi, na kila Muislam ajue haki ya mwili wake kwake, kuupa chakula na mazoezi, lakini pia haki ya kuiliwaza nafsi yake kwa aina mbali mbali za starehe za halali, na haki ya mke wake ya kumtunza na kuishi nae kwa wema, na haki ya mtoto wake ya kumlea na kumuelekeza na kuwa mpole kwake, na haki ya jamii kwa kufanya kila lenye maslahi katika jamii, kama vile anavyotambua haki ya Allah ya kumpwekesha na kumtii.

UISLAMU UNAYABOMOA (KUYAFUTA) YALIYOKUWA KABLA YAKE.

Na katika fadhila za Allah na Rehema zake ni pale alipoufanya Uislam unayabomoa yote yaliyo kabla yake, miongoni mwa madhambi na maasi mbali mbali, kwa hivyo kafiri akisilimu tu basi Allah humsamehe kila kosa alilotenda zama za ukafiri wake, na kuwa msafi hana dhambi yoyote.

Na mlango wa kutubu katika Uislam uko wazi hata kama huyu mja Muislam madhambi yake ni mengi mno, na mahitaji ya binadamu ya kutubu ni endelevu, kwa vile kila binadamu hufanya makosa, na mtu mwema katika wanaofanya makosa ni Yule anaetubia baada ya kufanya kosa. kama alivyosema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake-. Na kwa vile binadamu hana kinga inayomzuia kufanya madhambi, hakika Allah amemfungulia mlango wa kutubu, na amemwamrisha kufanya hivyo anapofanya kosa.

VIPI TUNAINGIA KATIKA UISLAM?

Na baada ya kujua utukufu wa dini ya kiislam, na kwamba hiyo ndio njia pekee ya kuokoka mbele ya Allah- mtukufu- na kwamba kuingia katika Uislam ni jambo la lazima kwa kila mtu, na kwamba hakuna njia ya kuingia peponi na kuokoka na moto siku ya kiama isipokuwa kwa kuingia katika Uislam, na jawabu la hilo ni kwamba ukitaka kuingia katika uislam ni juu yako tu kufanya haya:

Kuamini kwamba **hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa allah, na kwamba muhammad ni mjumbe wa allah**, na utamke hayo kwa ulimi wako, kisha uanze kujifunza sheria za kiislam na kuzitekeleza, mfano: kuswali nk. Na vitabu vya kujifunza hayo vipo vingi katika maktaba mbali mbali na vituo vya kiislam.